

# Nahodha wa meli yetu wenyewe?

## Maoni ya wananchi kuhusu ushiriki na maandamano

## 1. Utangulizi

Demokrasia ina maana pana zaidi ya chaguzi. Inahusisha pia kutoa fursa kwa wananchi kushiriki kwenye maamuzi muhimu ambayo yanagusa maisha yao, pamoja na kulinda haki za msingi kama vile uhuru wa kutoa maoni na uhuru wa kujumuika. Haki ya wananchi kufanya maandamano ya amani kama njia ya kuonesha kutoridhika kwao ni kitu muhimu kwenye jamii yoyote yenye demokrasia thabiti. Katika nchi nyingi, maandamano hayo ni kitu cha kawaida – aghalabu (mara kwa mara) kwa kiwango kidogo lakini mara chache hujumuisha watu zaidi ya milioni moja[1].

Nchini Tanzania hakuna utamaduni wa wananchi kuandamana mitaani kuonesha kutoridhika na jambo fulani, badala yake maandamano ya uhamasishaji kwenye maswala mbalimbali ya kijamii au kuadhimisha siku muhimu za kitaifa na kimataifa ni jambo la kawaida. Mara nyingi, maandamano ya aina hii huandaliwa au kuungwa mkono na serikali, lakini maandamano ya ghafla hutokea mara chache panapokuwa na malalamiko na fursa ya kushawishi jambo fulani.

Miaka ya hivi karibuni kumekuwa na majaribio makubwa mawili ya kuhamasisha maandamano dhidi ya serikali nchini Tanzania. Jaribio la kwanza lililojulikana kama UKUTA[2] lilihamasishwa na vyama vya upinzani kwa lengo la kufanya maandamano mwezi Septemba mwaka 2016. Jaribio la pili lililojulikana kama “maandamano ya Mange” lilihamasishwa na mwanaharakati wa kwenye mitandao ya kijamii anayeishi nchini Marekani, kwa lengo la kufanya maandamano mwezi Aprili 26, mwaka 2018. Kiuhalisia,

1 Kwa mfano wiki ya tarehe 23-29 Aprili mwaka 2018, maandamano ya amani yalifanyika nchini Malawi, Hispania, Armenia, Nicaragua na Afrika Kusini, kati ya sehemu nyingine nyingi.
2 Umoja wa Kupinga Udikteta Tanzania (Alliance Against Dictatorship in Tanzania

Muhtasari huu umeandikwa na umeandaliwa na Twaweza East Africa.

S.L.P 38342, Dar es Salaam, Tanzania. +255 22 266 4301 | info@twaweza.org | www.twaweza.org/sauti



Twaweza ni sisi

maandamano haya hayakufanyika, lakini matukio yote mawili yalikuwa na athari fulani kwenye hali ya kisiasa nchini Tanzania.

Muhtasari huu unawasilisha maoni ya wananchi kuhusu ushiriki na maandamano, kinadharia na kivitendo. Wananchi wanaelewa nini kuhusu "ushiriki", na kwa kiwango gani wanashiriki kwenye mikutano ya hadhara? Je, wananchi wanafikiri wanawezaje kutoa maoni na malalamiko yao kwa serikali? Je, ni kwa kiasi gani wananchi wako tayari kushiriki kwenye maandamano kuhusu masuala yanayowagusa, na je, wanaunga mkono uamuzi wa serikali wa kuzuia mikutano ya hadhara ya kisiasa? Na mwisho, kwa kutumia takwimu zilizokusanywa wiki mbili kabla ya Aprili 25, wananchi walikuwa na maoni gani kuhusu maandamano yaliyoandaliwa – je, walifahamu kuhusu maandamano hayo? Je, walipanga kuyapinga au kuyaunga mkono? Na je, walipanga kushiriki?

Takwimu za muhtasari huu zinatokana na utafiti wa Sauti za Wananchi. *Sauti za Wananchi* ni utafiti wa kwanza barani Afrika wenye uwakilishi wa kitaifa unaotumia simu za mikononi. Una uwakilishi wa Tanzania Bara pekee. Zanzibar haihusiki kwenye matokeo haya. Taarifa kuhusu mbinu za utafiti huu zinapatikana kupitia www.twaweza.org/sauti. Takwimu za muhtasari huu zilikusanywa kutoka kwa wahojiwa 1,241 kutoka awamu ya 27 ya kundi la pili la Sauti za Wananchi, zilikusanywa kati ya tarehe 15 na 24 ya mwezi Aprili mwaka 2018.

Matokeo muhimu ni:

- Wananchi wanaeleza maana ya ushiriki kama kuhudhuria mikutano na kushirikishwa kwenye kufanya maamuzi.
- Wananchi 7 kati ya 10 wanasema walihudhuria mikutano ya umma iliyoitishwa na serikali ya mtaa mwaka uliopita.
- Wanaume wana uwezekano mkubwa kuliko wanawake wa kuhudhuria mikutano ya umma na kuzungumza wakiwa kwenye mikutano hiyo.
- Wananchi wengi wanasema kwenda moja kwa moja kwenye ofisi za serikali ndio njia kuu ya kuwasilisha mahitaji yao kwa serikali.
- Wananchi 2 kati ya 3 wanasema hawana uwezekano wa kushiriki kwenye maandamano.
- Wananchi 5 kati ya 10 wanakubali kuzuiwa kwa mikutano ya kisiasa, 4 kati ya 10 hawakubali.
- Mwananchi 1 kati ya 4 alikuwa anafahamu kuhusu maandamano yaliyopangwa kufanyika tarehe 26 Aprili, 2018.
- Wananchi wachache sana (2%) wanaweza kumtambua vizuri Mange Kimambi kama mhamasishaji mkuu wa maandamano yaliyopangwa.
- Wananchi 4 kati ya 10 waliunga mkono maandamano yaliyopangwa, miongoni mwa wale waliokuwa na taarifa hizo na wale ambao walipewa maelezo mafupi kuhusu maandamano hayo wakati wa mahojiano.
- Wananchi 2 kati ya 10 walisema walikuwa na uwezekano wa kushiriki kwenye maandamano ya tarehe 26 Aprili.
- Uungaji mkono wa maandamano ya tarehe 26 Aprili mwaka 2018 ulikuwa mkubwa mara mbili zaidi ya uungaji mkono wa maandamano ya UKUTA mwaka 2016.


# 2. Mambo Tisa muhimu kuhusu ushiriki wa wananchi nchini Tanzania

## Jambo la 1: Wananchi wanaeleza maana ya "ushiriki" kama kuhudhuria kwenye mikutano na kushirikishwa katika kufanya maamuzi

Nusu ya wananchi (53%) wanataja kushiriki kwenye mikutano na kufanya maamuzi kama sehemu muhimu ya uelewa wao kuhusu ushiriki wa raia. Wananchi 3 kati ya 10 pia wametaja kujitolea nguvu kazi (31%) au kutoa michango ya hiari ya fedha kwa serikali (29%). Kupiga kura wakati wa chaguzi imetajwa na wananchi wachache mno (2%).

**Kielelezo cha 1: Ushiriki wa raia kwenye serikali una maana gani kwako?[3]**

*(jibu zaidi ya moja linaruhusiwa)*




**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa Sauti za Wananchi, Awamu ya 27 (Aprili 2018)

*Msingi: wahojiwa wote (1,241)*

## Jambo la 2: Wananchi saba kati ya kumi wanasema walihudhuria mkutano wa hadhara ulioitishwa na serikali ya mtaa mwaka jana


Wananchi saba kati ya kumi (70%) wanasema kuwa walihudhuria angalau mkutano mmoja ulioitishwa na serikali ya mtaa katika kipindi cha miezi kumi na miwili iliyopita. Wananchi wanne kati ya kumi (40%) wanasema waliuliza swali au walitoa hoja wakati wa mkutano huo.

Mahudhurio kwenye mikutano ya hadhara iliyoandaliwa na serikali za mitaa ni makubwa miongoni mwa wanaume (78%) kuliko wanawake (61%), lakini tofauti kubwa inaonekana kwenye uchangiaji katika mikutano hiyo: wanaume (53%) wana uwezekano mara mbili zaidi ya wanawake (27%) kusema wamezungumza kwenye mikutano hiyo.

Vilevile kuna tofauti ya mahudhurio baina ya wananchi waishio maeneo ya vijijini (75%) na mijini (59%), na wananchi wenye umri wa zaidi ya miaka 40 (77-78%) ikilinganishwa na vijana (18-29) (60%). Wananchi wenye elimu ya msingi (75%) wana uwezekano mkubwa wa kuhudhuria mikutano ikilinganishwa na wasiokuwa na elimu (59%) au wenye elimu ya juu (64%).

3 Jumla ya asilimia zote zinaweza zisifike 100% kutokana na makadirio.

**Kielelezo cha 2: Je, umehudhuria mkutano wowote wa kijiji/eneo ulioitishwa na mamlaka za serikali za mitaa miezi 12 iliyopita? Je, uliuliza swali/kuibua hoja?**




**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa Sauti za Wananchi, Awamu ya 27 (Aprili 2018)
Msingi: wahojiwa wote (1,241)

Mada zinazojadiliwa sana kwenye mikutano hii ni huduma za kijamii, zikiwemo shule (35% ya wananchi wamesema hivyo), maji (16%) na afya (15%). Pia, maswala mengine ya kiutawala yanajadiliwa kwa mapana, yakiwemo maendeleo ya kijiji/miundombinu (21%), bajeti ya kijiji (18%), polisi jamii (13%) na usafi (12%) (haijaoneshwa kwenye majedwali).


Sababu kuu ya watu **kutohudhuria** mikutano ni kwamba wametingwa na kazi (39%), ikifuatiwa na hisia kuwa kuhudhuria hakuleti mafanikio makubwa (23%) (haijaonesha kwenye majedwali).

## Jambo la 3: Wananchi wengi wanataja kutembelea ofisi za serikali kama njia kuu wanayoweza kuwasilisha maombi yao

Wananchi nane kati ya kumi (81%) wanataja kutembelea ofisi za serikali kuu au serikali za mitaa kama moja kati ya njia kuu tatu za kuwasilisha maombi yao, kuliko njia nyingine yoyote. Njia nyingine zilizotajwa ni kupitia wawakilishi wa vijiji ambapo wananchi wawili kati ya kumi (18%) wametaja njia hiyo, na idadi sawa na hiyo wametaja kuhudhuria mabaraza (mijadala ya hadhara) (17%) au kupitia kwa viongozi wao wa nyumba kumi (17%). Ni mwananchi mmoja tu kati ya kumi (10%) aliyeataja kutumia vyombo vya habari kama njia ya kuwasilisha maombi/maoni kwa serikali.

**Kielelezo cha 3: Je, unaweza kunitajia mpaka njia tatu unazotumia kama mwananchi, kuwasilisha mahitaji yako kwa serikali?**


*(majibu mpaka matatu yanaruhusiwa)*




**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa Sauti za Wananchi, Awamu ya 27 (Aprili 2018)
Msingi: wahojiwa wote 1,241

Karibu wananchi wote wanasema wangekuwa tayari kuhudhuria mkutano wa kijamii (96%) au kujiunga na wenzao kuibua hoja (97%), japokuwa idadi pungufu ya hiyo (71% na 44%) hufanya hivyo. Tofauti hii ni kubwa zaidi linapokuja suala la kuwasiliana na vyombo vya habari; 89% wanasema wangekuwa tayari kufanya hivyo lakini ni 5% pekee walifanya hivyo. Idadi ndogo (2%) wanasema wangekuwa tayari kutumia nguvu kwa ajili ya mambo ya kisiasa na idadi kama hiyo (1%) wanasema walifanya hivyo mwaka uliopita.

**Kielelezo cha 4: Je, wewe ungefanya nini kati ya vitu vifuatavyo? Je, umefanya hivyo mwaka uliopita?**





**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa Sauti za Wananchi, Awamu ya 27 (Aprili 2018)
Msingi: wahojiwa wote (1,241)

## Jambo la 4: Wananchi wawili kati ya watatu hawako tayari kushiriki kwenye maandamano

Idadi kubwa ya wananchi (65%) wanasema hawako tayari kutumia njia ya maandamano kuishinikiza serikali katika mambo yasiyowaridhisha. Kwa upande mwingine, mwananchi mmoja kati ya wanne (27%) ana uwezekanao wa kushiriki kwenye maandamano.

Ikilinganishwa na takwimu za mwaka 2016, idadi ya wanaosema wana uwezekano wa kushiriki imeshuka kidogo sana (kutoka 29% mpaka 27%) wakati ambao wanasema hawana uwezekano wa kushiriki imeongezeka (kutoka 50% mpaka 65%).

**Kielelezo cha 5: Je, una uwezekano wa kushiriki kwenye maandamano kuhusu jambo lisilokupendeza?**





**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa Sauti za Wananchi, Awamu ya 27 (Aprili 2018) na Awamu ya 11 (Agosti 2016)
Msingi: Wahojiwa wote (1,602 mwaka 2016; 1,241 mwaka 2018)

Utayari wa kushiriki kwenye maandamano unatofautiana kidogo baina ya makundi mbalimbali. Hakuna tofauti kwenye mitazamo ya wanawake na wanaume, lakini wale wanaoishi maeneo ya vijijini wanasema wana uwezekano zaidi wa kushiriki (29%) kuliko wale wa maeneo ya mijini (23%).

Kuna tofauti ndogo kati ya makundi ya rika mbalimbali: vijana (34%) wana uwezekano mara mbili zaidi ya wazee (18%) kusema wangeshiriki. Japokuwa hakuna tofauti kubwa baina ya makundi mbalimbali kwa vigezo vya kiuchumi (masikini na wasiokuwa masikini), wale masikini zaidi wana uwezekano mkubwa kuliko wasiokuwa masikini katika kushiriki maandamano (haijaonesha kwenye majedwali).

Tofauti inayojitokeza dhahiri ni kati ya wafuasi wa chama tawala na wafuasi wa vyama vya upinzani. Karibu wafuasi watano kati ya kumi wa vyama vya upinzani (45%) wanasema wana uwezekano wa kushiriki maandamano, ukilinganisha na wafuasi takriban wawili kati ya kumi wa chama tawala (24%). Wananchi wawili kati ya kumi wasio wafuasi wa chama chochote (22%) wanasema wangekuwa na uwezekano wa kushiriki.

**Kielelezo cha 6: Je, una uwezekano kiasi gani wa kushiriki wenye maandamano kuhusu jambo usilolipenda?**





**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa Sauti za Wananchi, Awamu ya 27 (Aprili 2018)
Msingi: wahojiwa wote (1,241)

Sababu kuu ya utayari wa kushiriki kwenye maandamano ni kwamba maandamano yanasaidia kushinikiza serikali kulinda haki za raia (*kupata haki zangu* 14%).

Sababu kubwa ya kutokuwa tayari kushiriki ni wasiwasi kuwa maandamano yanaweza kusababisha vurugu au uvunjifu wa amani (44%), ikifuatiwa na mtizamo kwamba maandamano siyo njia sahihi ya kutatua mifarakano (20%). Idadi ndogo pia wanasema hawana uwezekano wa kushiriki kutokana na hofu ya kupigwa na polisi (5%) au watu wengine (4%), kukamatwa (2%), au kwa sababu serikali imezuia maandamano (3%).

**Kielelezo cha 7: Kwanini una/hauna uwezekano wa kushiriki kwenye maandamano kuhusu jambo ambalo halikufurahishi?**

*(jibu zaidi ya moja linaruhusiwa)*




**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa Sauti za Wananchi, Awamu ya 27 (Aprili 2018)
Msingi: wahojiwa wote (1,241)


## Jambo la 5: Wananchi watano kati ya kumi wanakubali kuzuiwa kwa mikutano ya kisiasa, na wanne kati ya kumi hawakubali

Nusu ya wananchi (48%) wanaunga mkono uamuzi wa serikali wa kukataza maandamano na mikutano ya kisiasa kwa wanachama na viongozi nje ya majimbo yao, ikilinganishwa na wananchi wanne kati ya kumi (40%) wanaopinga uamuzi huo.

Vijana (41%) wana uwezekano mdogo kuliko wazee (60%) wa kukubali katazo hilo. Na wafuasi wa chama tawala (60%) wanakubaliana na zuio hilo kwa idadi kubwa zaidi kuliko wafuasi wa vyama vya upinzani (18%). Ni vema pia ikafahamika kuwa zaidi ya robo ya wafuasi wa chama tawala (27%) hawakubaliani na katazo hilo.

Wananchi kutoka maeneo ya vijijini (45%) wana uwezekano kiasi wa kuunga mkono uamuzi wa serikali kuliko wa maeneo ya mijini (52%), wakati wananchi wasiokuwa na elimu wana uwezekano mkubwa kiasi (53%) kuliko waliokuwa na elimu ya juu (46%) wa kuunga mkono katazo hilo.

**Kielelezo cha 8: Kwa kiwango gani unakubaliana na uamuzi wa serikali wa kuzuia maandamano na mikutano ya kisiasa?**





**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa Sauti za Wananchi, Awamu ya 27 (Aprili 2018)
Msingi: wahojiwa wote (1,241)

## Jambo la 6: Mwananchi mmoja kati ya wanne alikuwa amesikia kuhusu maandamano yaliyopangwa kufanyika Aprili 26, mwaka 2018

Mwananchi mmoja kati ya wanne (25%) alikuwa anafahamu kwa undani au kiasi kuhusu maandamano yaliyopangwa kufanyika Aprili 26, 2018. Idadi hii (25%) inajumuisha wananchi wachache (6%) waliofahamu kwa undani kuhusu maandamano yaliyopangwa, na wananchi wengi zaidi (19%) waliofahamu kiasi kuhusu maandamano yaliyopangwa.

Uelewa kuhusu maandamano yaliyopangwa ulikuwa mkubwa kidogo miongoni mwa wanaume (27%) kuliko wanawake (23%). Lakini ulikuwa mkubwa mara tatu zaidi miongoni mwa wakazi wa maeneo ya mijini (43%) kuliko maeneo ya vijijini (15%) na mara tano zaidi miongoni mwa wananchi wasiokuwa masikini (46%) ukilinganisha na wananchi masikini (9%).


**Kielelezo cha 9: Je, una taarifa za wito wa kushiriki kwenye maandamano ya nchi nzima Aprili 26, mwaka 2018?**




**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa Sauti za Wananchi, Awamu ya 27 (Aprili 2018)
Msingi: wahojiwa wote (1,241)

Miongoni mwa wananchi waliohojiwa, ni wachache sana (2%) waliweza kumtambua mwanaharakati wa kwenye mitandao ya kijamii anayeishi nchini Marekani aitwaye Mange Kimambi kama mhamasishaji mkuu wa maandamano yaliyopangwa, na wananchi wachache zaidi (1%) wanasema wanamfuata Mange Kimambi kwenye mitandao ya kijamii.

**Kielelezo cha 10: Uelewa wa wananchi kuhusu maandamano na Mange Kimambi**




**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa Sauti za Wananchi, Awamu ya 27 (Aprili 2018)
Msingi: wahojiwa wote (1,241)

Wananchi waliofahamu kuhusu maandamano yaliyopangwa, walitaja sababu kuu nne za maandamano hayo. Nusu yao (54%) walisema maandamano yameandaliwa kuonesha kutoridhika na uongozi wa nchi wakati wananchi watatu kati ya kumi (30%) walisema vitendo vya serikali na mamlaka zake kuminya uhuru na haki mbalimbali ndiyo sababu ya maandamano

hayo. Wengine walisema maandamano yalihusu uendeshaji mbaya wa uchumi (17%) au kupinga mauaji yanayodaiwa kufanywa na serikali (12%) (haijaoneshwa kwenye majedwali).

## Jambo la 7: Wananchi wanne kati ya kumi wanaunga mkono maandamano yaliyopangwa

Baada ya kusoma maelezo mafupi kuhusu maandamano yaliyoandaliwa na malengo yake[4], wananchi wanne kati ya kumi (42%) walisema wanaunga mkono maandamano yaliyopangwa kufanyika Aprili 26.


Uungaji mkono ulikuwa mkubwa miongoni mwa makundi ambayo takwimu zetu za nyuma zinaonesha mara nyingi huunga mkono chama tawala: waishio maeneo ya vijijini (45%), kwa mfano, waliunga mkono zaidi maandamano kuliko wale wa maeneo ya mijini (36%), na wananchi masikini (48%) kuliko wasiokuwa masikini (38%) (haijaonesha kwenye majedwali). Hata hivyo, uungaji mkono ulikuwa mkubwa miongoni mwa vijana (48%) ikilinganishwa na wazee (29%).

Wafuasi wa vyama vya upinzani wana uwezekano mkubwa (74%) wa kuunga mkono maandamano kuliko wafuasi wa chama tawala (32%). Hakuna tofauti ya kuunga mkono maandamano kati ya wale waliokuwa tayari na taarifa za mipango hiyo (42%) na wale waliokuwa hawana taarifa hizo kabla (43%).

---

4 “Kuna jitihada zinaendelea za kuandaa maandamano ya amani nchi nzima Aprili 26, 2018 ya kupinga uongozi mbaya wa serikali ya awamu ya tano. Malalamiko makubwa ni kuzuiwa kwa uhuru wa kuzungumza, kukosekana kwa ajira na hali mbaya ya uchumi, na mauaji yanayofanywa kwa makusudi kinyume cha sheria. Mahitaji yao ni tume huru ya uchaguzi, katiba mpya, na Rais wa Tanzania na Zanzibar kujiuzulu.” *Maelezo haya yaliandaliwa na Twaweza kwa kutumia taarifa kutoka kwenye akaunti za mitandao ya kijamii za Mange Kimambi.*

**Kielelezo cha 11: Kwa kufahamu malengo ya maandamano ya Aprili 26, je, unayaunga mkono?**





**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa Sauti za Wananchi, Awamu ya 27 (Aprili 2018)
Msingi: wahojiwa wote (1,241)

Mwananchi mmoja kati ya wanne (25%) alisema anaunga mkono maandamano yaliyopangwa kwa sababu serikali au polisi wanakiuka haki za raia, na idadi kubwa nyingine walitaja hali ngumu ya uchumi (20%) au kutokuheshimiwa kwa uhuru wa maoni (19%).

Wananchi watatu kati ya kumi (32%) walisema wanapinga maandamano kwa sababu ya hofu ya kutokea vurugu, wakati wengine walisema hawakuona sababu ya kuandamana kwa kuwa serikali inafanya vizuri (24%).

**Kielelezo cha 12: Kwa nini unaunga/hauungi mkono maandamano haya?**
*(jibu zaidi ya moja linaruhusiwa)*





**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa Sauti za Wananchi, Awamu ya 27 (Aprili 2018)
Msingi: wahojiwa wote (1,241)

## Jambo la 8: Wananchi wawili kati ya kumi walisema walikuwa na uwezekano wa kushiriki kwenye maandamano ya Aprili 26.

Wananchi wawili kati ya kumi (21%) walisema *walikuwa* na uwezekano wa kushiriki kwenye maandamano ya Aprili 26. Wananchi saba kati ya kumi (73%) walisema *hawakuwa* na uwezekano wa kushiriki.

Wananchi masikini (25%) na vijana (24%) na wasio na elimu (24%) walikuwa na uwezekano zaidi kuliko wasio masikini (17%) na wazee (14%) na wenye elimu ya juu (17%) kusema kuwa walikuwa na uwezekano wa kushiriki kwenye maandamano. Hakukuwa na tofauti kubwa kati ya wanawake na wanaume, au kati ya maeneo ya mijini na vijijini.

**Kielelezo cha 13: Je, una uwezekano kiasi gani wa kushiriki kwenye maandamano ya Aprili 26?**





**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa Sauti za Wananchi, Awamu ya 27 (Aprili 2018)
Msingi: wahojiwa wote (1,241)

Sababu kuu iliyotolewa na wale waliosema kuwa wangeshiriki ilikuwa ni kuunga mkono uhuru wa kutoa maoni (13%) na kutoridhishwa na uongozi wa awamu hii (12%).

Sababu kuu iliyotolewa ya kutoshiriki ilikuwa ni wasiwasi wa kutokea vurugu (51%), kuunga mkono serikali (18%) na hofu ya kujeruhiwa, mabomu ya machozi au kukamatwa (18%).

**Kielelezo cha 14: Kwanini una/hauna uwezekano wa kushiriki?**




**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa Sauti za Wananchi, Awamu ya 27 (Aprili 2018)
Msingi: wahojiwa wote (1,241) (jibu zaidi ya moja linaruhusiwa)

## Jambo la 9: Uungaji mkono wa maandamano ya Aprili 26 ulikuwa mkubwa mara mbili zaidi ya uungaji mkono wa maandamano ya UKUTA mwaka 2016

Japokuwa uungaji mkono wa maandamano kiujumla haujabadilika sana tangu mwaka 2016 (29% mpaka 27% mwaka 2018), uungaji mkono wa maandamano ya Aprili 26 ulikuwa mkubwa kuliko wa maandamano ya UKUTA Septemba mwaka 2016.


Wale wanaosema hawana uwezekano wa kushiriki kwenye maandamano yoyote wameongezeka kutoka asilimia 50 mwaka 2016 mpaka asilimia 65 mwaka 2018.

Tathmini ya wiki mbili kabla ya tarehe ya maandamano inaonesha kuwa ufahamu kuhusu maandamano ya Mange ya Aprili 26 ulikuwa mkubwa zaidi (25%) ikilinganishwa na ufahamu wa maandamano ya UKUTA (16%).

Uungaji mkono wa maandamano ya mwaka 2018 ulikuwa mkubwa kuliko maandamano ya mwaka 2016: wananchi wanne kati ya kumi (42%) mwaka 2018, ukilinganisha na wananchi wawili kati ya kumi (18%) mwaka 2016.

Vilevile, mara mbili zaidi ya wananchi walisema walikuwa na uwezekano wa kushiriki kwenye maandamano ya mwaka 2018 (21%) kuliko mwaka 2016 (9%).

**Kielelezo cha 15: Uelewa wa wananchi na uungaji mkono wa maandamano yaliyopangwa Septemba 2016 na Aprili 2018:**




**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa Sauti za Wananchi, Awamu ya 27 (Aprili 2018)
Msingi: wahojiwa wote (1,241)

Hatimaye, maandamano ya Aprili 26 hayakufanyika kama yalivyopangwa.

# 3. Hitimisho

Je, huenda watanzania hawapendi kushiriki katika masuala yanayowahusu? Hili linaweza kuwa moja ya masuala muhimu kuibuliwa na muhtasari huu. Wananchi wachache kwa hiari wametaja maandamano kama njia ya kufikisha malalamiko yao kwa serikali. Idadi kubwa ya wananchi wanasema hawako tayari kushiriki kwenye maandamano kuhusu jambo lolote lisilowapendeza – ikiwemo idadi kubwa ya wafuasi wa vyama vya upinzani. Na wananchi wengi zaidi wanaunga mkono serikali kukataza mikutano na maandamano ya kisiasa kuliko wale wanaopinga. Hitimisho hili bila shaka linaweza kuonesha wazi sababu ya kutokufanyika kwa maandamano ya April 26 mwaka 2018 kama yalivyokuwa yamepangwa.

Kuna sababu nyingine ambazo zimetajwa kusababisha watu kutojitokeza kwenye maandamano. Ikiwemo hofu iliyotajwa na wananchi kuwa maandamano yangeweza kusababisha vurugu na kwa kushiriki kwao kungeweza kuhatarisha maisha yao. Hata hivyo, matokeo ya muhtasari huu yafaa kutiliwa maanani kwani yanatoa mwanga kuhusu changamoto iliyopo ya kuandaa maandamano nchini Tanzania.

Kwanza, kuhamasisha idadi kubwa ya watu si jambo rahisi. Ni 6% pekee ya wananchi ambao walikuwa na taarifa za uhakika kuhusu maandamano yaliyopangwa, na 2% pekee waliweza kumtambua kwa usahihi Mange Kimambi kama mhamasishaji. Katika muktadha huu, kuandaa maandamano kutumia mitandao ya kijamii inaonekana imeathiri uwezekano wa maandamano kufanyika kiuhalisia.

Pili, kuna tofauti kati ya ufahamu wa maandamano yaliyopangwa na uungaji mkono wa maandamano hayo. Wanawake, watu masikini na wale wanaoishi maeneo ya vijijini wote walikuwa na uwezekano mdogo wa kufahamu kuhusu maandamano hayo kuliko wanaume, wasiokua masikini na wale waishio maeneo ya mijini. Lakini wale ambao hawakuwa wakifahamu sana kuhusu maandamano hayo ndiyo waliokuwa tayari zaidi kusema wangeyaunga mkono. Kwa maneno mengine, makundi kwenye jamii ambayo hayako karibu sana na vyombo vya habari (ikiwemo mitandao ya kijamii) ni makundi ambayo yangekuwa na uwezekano mkubwa wa kushiriki kwenye maandamano iwapo wangepata taarifa.

Tatu, sababu kubwa ambayo wananchi wanataja ya kupinga au kutotaka kushiriki kwenye maandamano kwa ujumla na maandamano ya Aprili 26 – ni hofu ya vurugu. Ikiwemo hofu binafsi ya kukamatwa na kutaka kudumisha amani na utulivu. Inawezekana mtazamo walionao wananchi kuwa maandamano ni vurugu na hatari, ndio ulisababisha maandamano yaliyopangwa kutokufanyika.

Mwisho, takwimu zilizowasilishwa hapa pia zinaonesha dhahiri wananchi wanaunga mkono sababu za Mange Kimambi na wafuasi wake za kuhamasisha maandamano. Uungaji mkono wa maandamano ya April 26 mwaka 2018, ni mkubwa mara mbili zaidi ya ule wa maandamano ya UKUTA Agosti mwaka 2016, ambayo nayo yalihusu malalamiko yale yale (japokuwa hayakujikita

kwenye masuala maalum sana). Kama ilivyoelezwa hapo juu, wale ambao hawaungi mkono maandamano au ambao hawakuwa na uwezekano wa kushiriki walisema ni kwa ajili ya kuogopa vurugu kuliko kutofautiana na malengo ya mwaandaaji.

Wananchi wana malalamiko, lakini hawaoni kama maandamano ni njia sahihi zaidi ya kuyaibua. Hususani pale wanapoona ushiriki wao ungehatarisha usalama wao pamoja na amani ya nchi.